TANGAZO LA SERIKALI Na. 278 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 153)*

## SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MILIMA NA VYANZO VYA MAJI (MAREKEBISHO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI YA MWAKA 2021

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Hifadhi Ya Milima Na Vyanzo Vya Maji (Marekebisho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ya Mwaka 2021 na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo za Hifadhi Ya Milima Na Vyanzo Vya Maji za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi za Mwaka 2014 ambayo katika Sheria Ndogo hii itajulikana kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya Tangazo la Serikali Na.392 la Mwaka 2014

2. Kifungu cha 2 cha Sheria Ndogo Kuu kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza tafsiri ifuatayo;
"Chanzo cha Maji"; ni eneo lote panapoanza maji na eneo lote linalo hifadhi eneo hilo.

3. Kifungu cha 5 cha Sheria Ndogo Kuu kinafanyiwa marekebisho kwa kuongezewa kifungu kidogo cha (c) na (d)

5. (c) Ni marufuku kwa Mtu yeyote kuharibu vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kuendesha shughuli za kibinadamu katika maeneo yaliyotengwa na yasiyotengwa;

*Tangazo la Serikali Na. 278 (Linaendelea.)*

(d) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shillingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili yani faini na kifungo.

*Tangazo la Serikali Na. 278 (Linaendelea.)*

Mabadiriko haya yanasomeka pamoja na Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi iliyobandikwa kwenye Marekebisho ya Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ya mwaka 2019 kufuatia azimio lililopitishwa na mkutano wa halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 28/2/2020. Na Nembo hii inabandikwa:-

MISSANA K KWANGURA,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*NKASI*

SUMUNI ZENO MWANAKULYA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*NKASI*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
3 Machi, 2021

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi*